



Malaysia: Semina "Uhusiano kati ya Khilafah na Ulimwengu wa Malay" kufunga Kampeni ya Rajab 1444 H

(Imetafsiriwa)

KUALA LUMPUR, 19 Februari 2023 - Baada ya mwezi mmoja wa kufanya kampeni ya ukumbusho wa kuanguka Khilafah mnamo tarehe 28 Rajab 1342 Hijri, Hizb ut Tahrir/Malaysia imefunga kampeni kwa kufanya semina ya mseto inayojadili mada hiyo.

Mtaalamu wa historia ya Nusantara (Malay Archipelagos) kutoka Indonesia, Ustadh Nicko Pandawa, alialikwa kama mgeni maalum katika semina hiyo ambaye alitoa mada yake kwa kichwa "Khilafah na Ulimwengu wa Malay: Uhusiano wa Jihad katika Kuzuia Ukoloni wa Kimaghribi".

Ustadh Nicko pia ni mwelekezi wa filamu ya "Jejak Khilafah di Nusantara" (Nyayo za Khilafah huko Nusantara), filamu ambayo inazungumziwa sana nchini Indonesia, na pia ni mwandishi wa vitabu kadhaa vya kihistoria kuhusu uhusiano kati ya Nusantara na Khilafah.

Wanajopo wengine ni pamoja na Dkt. Tarmizi Salleh, Prof. Dkt. Muhammad Abu al-Ain na Ustadh Abdul Hakim Othman, kila mmoja aliwasilisha karatasi zenye kichwa: "Historia ya Uhusiano kati ya Ulimwengu wa Malay na Khilafah", "Kufichua Ajenda ya Magharibi ya Kuondo la Fikra ya Kiislamu huko Nusantara" na "Nusantara na Faradhi ya Kusimamisha Tena Khilafah" mtawalia.

Semina ilianza majira ya saa nne asubuhi na kumalizika majira ya saa saba mchana na alhamdulillah ilikwenda vizuri.

Miongoni mwa risalam muhimu zilizotolewa katika semina hii ni ufahamu ambao Waislamu wa Nusantara wanapaswa kuwa nao kuhusiana na ushahidi wenye nguvu na sahihi wa kihistoria, kwamba Khilafah na ulimwengu wa Malay ina uhusiano wa karibu wa haki na watawala wa Nusantara kwa jumla wanaitambua nafasi na mamlaka ya Khalifa kuwa ndiye kiongozi mkuu wa Waislamu wote duniani.

Kilicho muhimu zaidi kwa Waislamu kuzingatia na kukumbuka, hasa kuhusiana na mwezi wa kuanguka Khilafah, ambayo imekuwa ni historia ya giza kwa Waislamu, ni juu ya ufaradhi wa kusimamisha tena taasisi hii tukufu ya kisiasa kwa umakini.

Ni kwa njia hii pekee Waislamu wataweza kurudisha izza ya Uislamu, kuwaunganisha Waislamu, kuwashinda maadui wa Uislamu, kurudisha hadhi ya Umma huu na kuuregesha Uislamu kama dola kuu ya ulimwengu. Huu ndio ujumbe kutoka kwa kila mwajopo katika semina hii licha ya mada zilizojadiliwa.

Ijapokuwa mwezi wa Rajab umekwisha, juhudhi na miito ya Hizb ut Tahrir ya kusimamisha tena Khilafah Rashida kwa njia ya Utume hazitakwisha hadi Mwenyezi Mungu (swt) atimize ahadi yake.

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir

Malaysia